# Ujumbe wa Jenerali wa Mwaka Mpya 2025

Wapendwa marafiki zangu Waumini wa Jeshi la Wokovu,

Heri ya Mwaka Mpya! Neema na amani iwe kwa kila mmoja wenu kutoka kwa Mungu Baba yetu kupitia kwa Yesu Kristo Bwana wetu.

Tunapoanza mwaka 2025, nina shauku kuona jinsi Bwana atakavyotumia Compass, Mfumo wa Kazi wa Mkakati Duniani kote. Lengo lake ikiwa kuzingatia **watu**, **utume** na **urithi**, naamini kwamba Bwana atatuwezesha tukamilishe mambo makubwa katika jina lake tunapojitoa kuwa wanafunzi wake na kuendelea na kazi ya utume tuliyodhaminiwa. Sisi sote tuna sehemu ya kutimiza.

Mwaka huu vile vile tunaadhimisha miaka 160 toka Waanzilishi wetu, Catherine na William Booth, walipoanzisha kazi ya Jeshi la Wokovu. Wametuachia urithi wa jinsi gani. Kutangaza injili, kutafuta maisha ya utakatifu na hamu ya kupenda na kuwajali majirani zetu. Tunaposherehekea miaka 160 mwaka 2025, hebu tudhamirie kwamba sisi pia tutaacha urithi unaomheshimu Mungu, unaojenga Ufalme na kuhakikisha tunakabidhi chombo kinachostahili jina lake na utume.

Bila shaka, sijui mwaka mpya una maana gani kwako. Baadhi yenu mnaweza kuwa mnazindua mwaka mpya uliojaa shauku na matarajio. Wengine mnaweza kuwa

mnaingia katika mwaka 2025 mkiwa mnajisikia mna woga au wasiwasi kwa sababu ya mazingira ambayo ni halisi kwenu.

Bila kujali hali yako binafsi, kuchagua kutoa kipaumbele kwake Bwana na uhusiano wako na yeye ndiyo uamuzi bora zaidi utakaoufanya mwaka 2025.

Marafiki zangu, tunaweza kumwamini. Yeye hatatukatisha tamaa. Nilipokuwa kijana mdogo, nikikua katika Jeshi la Wokovu, tulikuwa tukiimba pambio hii:

*Ninaye rubani anayeniongoza usiku na mchana; kupita katika mawingu na mwanga wa jua namwamini, lije lolote.*

*Hatari zinaweza kutishia lakini mimi siogopi, nina ujasiri wote anapokuwa karibu, ninaye rubani anayeniongoza katika njia ya maisha.*

Hii ndiyo furaha ya uzoefu wa Kikristo. Ahadi hii kwamba Bwana mwenyewe yupo pamoja nasi, bila kujali mazingira yetu, bila kujali nafasi zetu, na anaahidi kuendelea kuwa mwaminifu kwetu.

Maombi yangu kwako ni kwamba maendeleo ya uhusiano wako na Yesu utabakia kuwa kipaumbele chako cha juu. Tunahitaji wanafunzi wa Yesu. Dunia inahitaji wanafunzi wa Yesu.

Tunapoanza mwaka huu mpya, hebu niwashirikisheni ahadi hii kutoka katika Maandiko, kutoka kwa barua ya Paulo kwa Warumi:

‘Basi Mungu wa tumaini na awajaze ninyi furaha yote na amani katika kuamini, mpate kuzidi sana kuwa na tumaini, katika nguvu za Roho Mtakatifu’ (Warumi 15:13).

Naomba Mungu awabariki.

**Lyndon Buckingham**
**Jenerali**